## USAID PROTECT inavyoendeleza mazingira,uhifadhi na utalii Tanzania

**Na Albano Midelo**




SHIRIKA la USAID kupitia mradi wake wa Promoting, Tanzania,Envronment Conservation and Tourism(PROTECT) limekuwa linaendeleza mazingira, uhifadhi na utalii hapa nchini lengo likiwa ni kupunguza uharibifu wa bioanuwi na kuimarisha uhifadhi wake.

Mwakilishi wa USAID PROTECT Thadeus Binamungu anabainisha kuwa hapa Tanzania shirika lake linakabiliana na mambo yanayotishia uhifadhi wa bioanuwai na kuzuia ukuaji wa utalii chini ya sekta binafsi.

Katika kutekeleza hilo Binamungu anasema USAID PROTECT inajikita katika kuwekeza mikakati itakayowezesha kujenga na

kuimarisha uwezo wa kuhifadhi bioanuwai kwa kuimarisha asasi mbalimbali ili ziweze kushiriki Zaidi katika michakato ya kuandaa na kuboresha sera.

Anasema PROTECT pia inasaidia kuimarisha uhifadhi wa bioanuwai na utalii,kuchangia kuongezeka kwa uwekezaji wa sekta binafsi Bna kupunguza uharibifu wa bioanuwa na kuimarisha uhifadhi wake kwenye maeneo ya mradi.

Katika kutekeleza kwa vitendo USAID PROTECT ilianza kutoa msaada katika Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii (CBCTC) kilichopo Likuyu Sekamaganga wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma.

Amesema msaada katika chuo hicho ulianza kutolewa na PROTECT kuanzia mwaka 2016 na kwamba hadi kufikia Juni 2018,Shirika hilo limetoa misaada ya vifaa vyenye thamani ya Zaidi ya shilingi milioni 46 hali ambayo imepunguza baadhi ya changamoto zinazokikabili chuo hicho.

Binamungu anaitaja misaada ambayo imetolewa kuwa ni kudurusu na kupitia mtaala wa kozi za askari wanyamapori wa vijiji(VGS) na viongozi wa Kamati za Maliasili za Vijiji ambapo mtaala umepitiwa na kuboreshwa kwa kuongeza fani nyingine ambazo hazikuwepo awali,pia muda wa mafunzo umeongezeka .

“Mafunzo kwa Askari wanyamapori wa vijiji muda umeongezwa toka toka wiki sita hadi miezi mitatu,mafunzo kwa viongozi wa serikali na wajumbe wa Kamati za Maliasili za Vijiji imeongezwa mwezi mmoja badala ya wiki mbili”,anasema Binamungu.



Hata hivyo amesema Shirika lake pia limeandaa mtaala wa mwaka mmoja wa kozi ya waongoza watalii katika chuo hicho ambapo mtaala huo umeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya NACTE na tayari umewasilishwa NACTE kwa ajili ya kuthibitishwa ili kozi hiyo iweze kuanzishwa chuoni CBCTC na kukiwezesha chuo hicho kusajiliwa.

Kwa mujibu wa Mwakilishi huyo wa PROTECT,misaada mingine ambayo imetolewa katika chuo hicho ni mafunzo ya kitaaluma kwa wakufunzi kwa kuwapatia mafunzo ya mbinu za kufundishia na matumizi ya mtaala ulioandaliwa kwa kuzingatia viwango vya NACTE,kuzingatia ubora katika utoaji mafunzo,sera,sheria na kanuni zinazohusiana na uhifadhi wa maliasili na miongozo ya matumizi ya ardhi kwa jamii zinazoishi kuzunguka maeneo ya hifadhi.

Binamungu anavitaja vifaa mbalimbali ambavyo PROTECT imevitoa katika chuo cha CBCTC Namtumbo kuwa ni kuwanunulia jenereta moja,viona mbali 10,GPS kumi,kompyuta mpakato tano,powerpoint mbili na vitabu 40 kwa ajili ya kozi ya waongoza watalii.





Kati ya vitabu hivyo,vitabu 12 ni vya wanyama wanyonyeshao,vitabu 12 vya ndege,vitabu 10 vya mimea na vitabu sita vya jamii ya mijusi na kwamba vifaa hivyo vimetolewa rasmi kwa ajili ya kusaidia na kurahisisha ufundishaji wa kozi ya waongoza watalii mara itakapoanzishwa katika chuo cha CBCTC Namtumbo.




Mkuu wa Chuo cha CBCTC Namtumbo Jane Nyau amethibitisha nyaraka,vitabu na vifaa vilivyotolewa na PROTECT kukabidhiwa rasmi na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii Meja

Jenerali Gaudence Milanzi sasa ni mstaafu katika mahafali ya chuo hicho.




Nyau anatoa shukrani za dhati kwa PROTECT kwa msaada wa vifaa hivyo ambao utasaidia kuboresha chuo hicho pamoja na kuanza kutoa kozi yam waka mmoja ya waongoza watalii ambayo inatarajiwa kutolewa kuanzia mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

“Ni matarajio yangu PROTECT wataendelea kutoa misaada mbalimbali kwa chuo hiki kwa kadri ya mahitaji na hivyo kukifanya kutimiza lengo lake la kuwa kituo bora cha utoaji mafunzo ya uhifadhi wa maliasili kwa jamii barani Afrika”,anasisitiza Nyau.

Akizungumzia matokeo tarajiwa ya mradi wa PROTECT,Afisa mawasiliano wa USAID PROTECT Symphrose Makungu anasema mradi umelenga kuboresha uhifadhi katika ngazi ya ikolojia kwa kuongeza ulinzi wa maliasili na kuuza ukuaji wa utalii.

Anasema matokeo ya mradi yatasaidia kuongeza uchumi na uhifadhi wa mazingira katika jamii mbalimbali na kuandaa mikakati ya kukabiliana na mambo hayo,kushawishi na kutekeleza sera zinazofaa ambazo zinaanisha ukuaji wa uchumi na uendelezaji wa malengo ya uhifadhi.

Makungu anazitaja shughuli za USAID PROTECT kuwa zimejikita Zaidi kwenye sera,utafiti na ushawishi ambapo mradi unaimarisha mazingira ya sera na utekelezaji wake ili kufanikisha uhifadhi wa bioanuwai na kukuza uchumi.

“Shughuli nyingine ni kujengea uwezo asasi za Tanzania wa kukabiliana na changamoto za sasa na za baadaye zinazohusiana na maliasili,kuingia mikataba na kufanya kazi kwa uwazi na uwajibikaji zaidi”,anasema Makungu.

Kulingana na Afisa mawasiliano huyo,mtazamo na mwelekeo wa USAID PROTECT ni uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta ya maliasili lengo ni kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika uhifadhi wa maliasili na uendelezaji wa utalii nchini Tanzania.

Takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2016,biashara ya utalii Tanzania ilichangia asilimia 14 ya pato la jumla la Taifa,ilichangia ajira milioni moja na nusu na kuchangia asilimia 25 ya fedha za kigeni.

Kutokana na umuhimu wa sekta ya utalii hapa nchini,ni muhimu kuendeleza mazingira,uhifadhi na utalii.Hivyo basi kutoweka kwa jamii muhimu za viumbe sio tu kutaleta maafa katika uhifadhi bali kunaathiri kwa kiasi kikubwa uimara wa uchumi.

**Mwandishi wa Makala haya ni mchangiaji wa gazeti hili,mawasiliano albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917**